

Sera ya Faragha
Tarehe ya usasisho wa mwisho: Julai 6, 2023

Sapien Labs (Maabara za Sapien) ni shirika la utafiti lisilo la faida (kibiashara) 501 (c) 3 lililoko Arlington, VA nchini Marekani lenye dhamira ya kuelewa na kuwezesha akili ya binadamu. Sera hii ya faragha inafanua jinsi Sapien Labs hutumia taarifa tunayokusanya kutoka kwako unapokamilisha tathmini ya Kiwango cha Afya ya Akili.

Kutambua Taarifa

Ufanyaji tathmini ya Kiwango cha Afya ya Akili hautakuhitaji kutoa taarifa zozote binafsi zinazoweza kukutambulisha. Mwishoni wa tafiti hii, ikiwa kama utapendelea kupokea ripoti yako ya kina itolewayo bure sambamba na alama yako ya jumla na muhtasari mfupi wa ripoti, basi utaombwa kushirikisha anwani ya barua pepe ili uweze kutumiwa nyaraka hizo. Jambo hili si lazima.

Matumizi ya Anwani ya Barua Pepe

Anwani yako ya barua pepe, ikiwa imetolewa, hutumiwa hasa kwa madhumuni ya kutuma ripoti ya kina kwako na pia inaweza kutumika kama kitambulisho cha kutathmini na kuweka kanuni ya tathmini nyingi zinazotoka katika anwani sawa ya barua pepe. Tunaweza pia kukutumia vikumbusho vya kila mwaka vya kukukumbusha kufanya tathmini ya Kiwango cha Afya ya Akili (MHQ) na mara kwa mara tunaweza kuwasiliana na wewe na kukualika kushiriki katika tafiti za ufuatiliaji ikiwa utakubaliana na hilo na kutupatia idhini ya kufanya hivyo. Anwani yako ya barua pepe haitasambazwa kwa washirika wowote wasiohusika wala kutumiwa kwa madhumuni mengine yoyote yale. Anwani yako ya barua pepe iliyohusika katika hatua yoyote ya tathmini hii, itafutwa ndani ya kipindi cha miaka 2 tangu tarehe ya uchukuaji wa tathmini na itahifadhiwa tu kama kitambulisho kilichowekewa usimbaji fiche.

Matumizi ya Taarifa

Majibu yote yaliyotolewa katika utafiti yanatumika kwa madhumuni ya utafiti wa kisayansi ya Sapien Labs na washirika wake wa utafiti pekee na hayatashirikishwa na wahusika wengine kwa madhumuni yoyote ya kibiashara. Taarifa itatunzwa na kuhifadhiwa kwa usalama kama sehemu ya kumbukumbu za utafiti za Sapien Labs kwa muda unaohitajika ili kutimiza madhumuni ya utafiti wa kisayansi.

Usimamizi na Uhamisho wa Taarifa

Taarifa zote na ushiriki wa ndani wa taarifa unadhibitiwa na wasimamizi walioteuliwa kwa ajili ya taarifa ya utafiti. Anwani za barua pepe zinaweza kuonwa na kufanyiwa kazi na watu hawa pekee na hazitatumwa kwa mtu mwingine yeyote. Taarifa zingine zote zinaweza kuhamishiwa kwa watafiti wa Sapien Labs na washirika wengine wa utafiti. Tunaweza pia kuhamisha, na kuhifadhi taarifa tunayokusanya kutoka kwako kama sehemu ya tathmini hii katika nchi nyingine jirani na nchi ambayo taarifa ilikusanywa hapo awali. Tunapohamisha taarifa yako hadi nchi nyingine, tatalinda taarifa kama ilivyofafanuliwa katika Sera hii ya Faragha na kutii mahitaji ya kisheria yanayotumika kutoa ulinzi wa kutosha kwa uhamishaji wa taarifa.

Kuomba Taarifa Yako

Iwapo hukutoa barua pepe ili kupokea ripoti ya kina ya tathmini, kwa kuwa hujulikani jina lako, hutaweza kuomba majibu yako kwa tathmini. Hata hivyo, Iwapo ulitoa barua pepe, unaweza kuomba taarifa yako ndani ya miaka 2 kuanzia tarehe ya kufanya tathmini kwa kutumia barua pepe hii info@sapienlabs.org. Tumia anwani ile ile ya barua pepe uliyotoa wakati wa kufanya jaribio, ikionyesha ombi lako pamoja na tarehe ya jaribio. Sapien Labs itatuma taarifa yako kwa anwani hii ya barua pepe ndani ya siku 30 baada ya ombi lako.